Mkulima Mbunifu

Jarida la Kilimo Endelevu Afrika Mashariki

TOLEO MAALUMU, 5

# Fahamu njia asili za kudhibiti visumbufu vya mbogamboga



***Uzalishaji wa mboga mara nyingi unahusisha matumizi ya viuatilifu vyenye kemikali. Baadhi ya wakulima hawawezi kumudu gharama kubwa za viuatilifu hivi, ambavyo visipotumika vizuri huweza kuleta madhara, kama kuharibu mazingira, mimea na kuathiri watumiaji wa mboga.***

Njia asilia za kudhibiti visumbufu hutumia dawa zinazotokana na mimea ambayo hupatikana katika maeneo ya wakulima. Matumizi ya dawa hizi ni njia mojawapo ya kuepuka dawa za viwandani ambazo huathiri udongo, mazingira na afya za watu na wanyama.

Madawa haya yasipotengenezwa vizuri na kutumiwa ipasavyo yanaweza yasifanye kazi ipasavyo na hivyo kuwa vigumu kuwashawishi wakulima kuzitumia.

Inashauriwa kutumia dawa hizi kama kinga kabla mashambulizi hayajashamiri kwani zinafanya kazi taratibu, hivyo ni vizuri kuzitumia kama kinga kuliko tiba.

SOMA ZAIDI NDANI

- MCHICHA
- NDULELE
- SAUMU
- PILIPILI KALI
- MAJIVU
- MFORI

Toleo hili limetayarishwa na kuchapishwa na ***Mkulima Mbunifu***

Mhariri: Erica Rugabandana, Mhariri Msaidizi: Flora Laanyuni, Mpangilio: Cathbert Msemo

Mkulima Mbunifu: S. L. P. 14402, Arusha, Sakina, Barabara ya Majengo, Jengo la Elerai.

www.mkulimambunifu.org, barua pepe: info@mkulimambunifu.org

Rununu +255717 266007, +255766841366

# Sifa za dawa za asili




- Upatikanaji wake uwe rahisi na isiwe na ushindani wa virutubisho na mazao.
- Iwe rahisi kutengeneza na isiyohitaji maandalizi ya kiteknolojia na isichukue muda mrefu kutengeneza.
- Matokeo yenye kuonekana. Mara nyingi dawa hizi hufukuza wadudu zaidi kuliko kuua.
- Unafuu wa gharama. Dawa hizi hupatikana bure ila utayarishaji wa dawa hizi lazima upimwe kulingana na gharama zitakazojitokeza kulingana na mgongano wa mazingira yakilinganishwa na madawa yaliyokwisha tengenezwa la sivyo wakulima wataendelea kutumia sumu. Uwezo wa kuua wadudu walengwa tu bila kudhuru viumbe hai marafiki.

## Zifuatazo ni baadhi ya dawa za asili na jinsi ya kutengeneza

### Majivu

- Weka majivu moja kwa moja kwenye mashina ya mimea michanga baada ya kuotesha ili kuzuia wadudu wakatao mimea michanga.
- Majivu huonyesha matokeo mazuri endapo yatachanganywa na mafuta ya taa kidogo.




### Pilipili kali

Hii ni moja ya dawa za asili ambazo zimekuwa zikitumika na kwa ufanisi mkubwa. Dawa hii inapotengenezwa na kutumika kwa umakini huwa na ufanisi mkubwa zaidi katika udhibiti wa wadudu na magonjwa.





#### Jinsi ya kutengeneza

- Chukua gramu 55 za pilipili.
- Katakata vipande vidogo vidogo kisha chemsha kwa dakika 20 kwenye maji ya lita tano.
- Chuja kisha ongeza maji lita 5

Dawa hii huua wadudu wenye ngozi ngumu (mbawa kavu) na laini kama vidukari, wadudu wa kabichi na wengineo.

### Vitunguu saumu

Dawa hii hutumika kufukuza wadudu kutokana na harufu yake.




#### Jinsi ya kutengeneza

- Chukua gramu 100 za vitunguu
- Twanga vilainike
- Changanya na maji lita mbili.
- Chuja kisha nyunyiza kwenye mimea.

Dawa hii pia inaweza kuchanganywa na mojawapo ya dawa za asili, ili kutoa harufu kali itakayofukuza wadudu.

### Tumbaku

- Tumia ugoro au chemsha miche 20 ya tumbaku.
- Dawa hii inazuia wadudu wanaoshambulia mahindi shambani, wadudu wanaokata miche, kupe, vidukari, viwavi na wengineo.

- Chukua gramu 500 za tumbaku, changanya maji lita nane na uchemshe. Chuja baada ya kupoa, ongeza maji lita nane tena na gramu 60 za sabuni ili kuongeza ubora.
- Ni muhimu kuwa na tahadhari kwa kuwa tumbaku ni sumu kwa binadamu na wanyama, hivyo weka mbali na wanyama wafugwao.

Inashauriwa kuvuna mazao siku 4-5 baada ya kunyunyiza aina hii ya dawa.




## Ndulele/ ndula

- Chukua matunda ya ndulele 30 au 40 haijalishi yameiva au mabichi.
- Katakata na uyakamue ili kupata juisi.
- Ongeza lita moja ya maji, koroga sawa sawa kisha chuja.
- Ongeza maji lita mbili.

Tumia lita moja ya dawa kwa lita 15 za Maji kisha nyunyiza mimea mara mbili kwa wiki.




## Mchicha (kwa ajili ya ukungu)

- Chukua kilo 1 ya mchicha.
- Twanga kisha loweka kwenye maji Lita moja.
- Acha ikae kwa saa 12.
- Ongeza sabuni gramu 20.
- Koroga ili sabuni iyeyuke.
- Kisha ongeza maji lita 2 na uchuje.

Tumia kwa uwiano wa 1:10 yaani lita 1 ya dawa kwa lita 10 za maji.




## Mchanganyiko wa mwarobaini

Majani ya mwarobaini ni kiuatilifu cha asili chenye uwezo wa kudhibiti wadudu kama vimamba, mbawakawa/ kombamwiko, panzi, Funza/viwavi, mbawakawa wa kijapani, nzige, wadudu wenye magamba laini, chawa/ vithiripi, fukusi, utitiri na nzi weupe.

- Ponda kilo 2 za majani ya mwarobaini na weka katika chombo chenye mfuniko.
- Ongeza lita 2 za maji, funika vizuri na uache kwa siku 3.
- Chuja kupata mchanganyiko wako.
- Chukua lita moja kutoka kwenye mchanganyiko wa lita mbili na uchanganye na lita 9 za maji.
- Ongeza mili lita10 za sabuni iliyoyeyushwa.
- Koroga vizuri na nyunyiza kwenye mimea iliyoathiriwa.




## Mchanganyiko wa mchaichai

Mchaichai una ufanisi mkubwa wa kuzuia magonjwa ya ukungu na bakteria kwenye mboga mboga.

- Ponda gramu 50 za mchaichai, uloweka ndani ya lita mbili za maji kwa usiku mzima.
- Chuja mchanganyiko huo na kuuweka moja kwa moja kwenye bomba la kunyunyiza (zidisha mchanganyiko wa maji na mchaichai kiasi cha mara mbili au tatu kulingana na wingi wa mazao yako).

Nyunyiza mchanganyiko huo mara moja kwa wiki. Rudia tena kama kuna ulazima.



## Majani ya basili/mfumbasi

Majani ya basili/mfumbasi yana ufanisi mkubwa dhidi ya viwavi, nzi wa matunda, utitiri mwekundu, utitiri mweupe, wadudu wenye magamba laini, kombamwiko wa madoa, magonjwa ya fangasi na minyoo fundo.

- Ponda gramu 50 za majani ya basili/mfumbasi na loweka ndani ya lita mbili za maji kwa usiku mzima.
- Tumia chujio kumimina mchanganyiko huo ndani ya bomba la kunyunyiza pamoja na mililita 10 za mchanganyiko wa sabuni na koroga vizuri.

Tumia mara moja kwa wiki, rudia tena kama kuna ulazima.




## Sabuni na maji

- Kata kipande kimoja cha sabuni.
- Yeyusha katika lita moja ya maji.
- Hifadhi mchanganyiko huo katika chombo maalumu.




**Muhimu:**

Mchanganyiko huu wa sabuni pia unafaa dhidi ya vimamba au inzi weupe, unapoyunyizwa.

## Kitunguu saumu

Kitunguu saumu pia kinaweza kuwa mbadala wa kudhibiti viwavi, nzi wa matunda, utitiri mwekundu, utitiri mweupe, wadudu wenye magamba laini, kombamwiko wa madoa, magonjwa ya fangasi na minyoo fundo.

- Menya kilo mbili za kitunguu saumu na uzitwange vizuri (tumia blenda ni vizuri zaidi).
- Ongeza mililita 500 za maji ili kusaidia kukamua juisi/mchanganyiko.
- Tumia chujio kupata mchanganyiko wa kitunguu saumu.
- Weka kwenye chupa au chombo maalumu na ongeza maji kutengeneza lita 10 za mchanganyiko.
- Weka mchanganyiko huo kwenye chombo kilichofunikwa. Weka alama kwenye chombo hicho.
- Kwenye mchanganyiko wa lita 10, toa lita moja na weka kwenye bomba la kunyunyiza, ongeza lita 15 za maji ili kukamilisha tanki zima, na ongeza mililita 10 za sabuni kimiminika.

Nyunyiza wakati wa asubuhi au jioni kwenye mimea iliyoathiriwa. Nyunyiza kila baada ya wiki moja. Mchanganyiko huo unaweza kutumika ndani ya miezi 3.

Jinsi ya kutengeneza mchanganyiko/mchapulo wa viuatilifu asili

Mchanganyiko huu unaweza kutumika kudhibiti wadudu wanaofyonza na kutafuna

Kata kata vipande vidogo vya mimea ifuatayo:

- Kilo 1 ya majani ya mwarobaini, gramu 500 za kitunguu swaumu, gramu 500 za tangawizi, mimea 5 ya mchaichai na majani mabichi 5 ya tumbaku.
- Chemsha mchanganyiko kwenye lita 20 za maji.
- Changanya wakati wa kuchemsha, ongeza vipande vya sabuni vilivyosagwa kwenye mchanganyiko huo.
- Baada ya kuchemsha, acha mchanganyiko huo upoe.
- Tumia chujio kuchuja mchanganyiko huo na kuweka kwenye chombo maalumu.
- Weka mililita 450 za kiuatilifu asili kwenye maji lita 16, nyunyiza wakati wa asubuhi au jioni kila baada ya wiki moja.

Mchanganyiko huo unaweza kutumika ndani ya miezi 3.

## Mkojo wa ng'ombe (mfori)

- Mkojo wa ng'ombe au wanyama wengine ukivundikwa vizuri kwa muda wa siku 10-14 unaweza kuwa kiua wadudu kizuri kwa ajili ya wadudu wengi waharibifu wa mimea
- Tengeneza mtaro wa kukinga mchanganyiko wa mkojo na kinyesi cha ng'ombe kutoka kwenye zizi
- Chimba shimo dogo kisha weka ndoo kukinga mkojo huo
- Hifadhi mchanganyiko huo ili uchachuke kwa muda wa siku 10-14
- Zimua kiasi 1 cha mkojo na maji 2 hadi 6 (1:2-1:6)
- Ongeza sabuni kidogo au majivu.
- Chuja vizuri tayari kwa kunyunyizia kwenye mimea kwa uwiano wa 2-6:15




***Makala hii ni kwa hisani ya http://www.sevia.biz/NJIA%20ASILI%20KUDHIBITI%20WADUDU%20SUMBUFU%20NA%20MAG ONJWA.pdf Tarehe 06/27/2018***

Haki zote zimehifadhiwa ©2024 *Mkulima Mbunifu*